# Usilahaishaji Lugha katika Intaneti kama Tisho kwa Umoja wa Kitaifa

*Mosol Kandagor*[1] na *Mahero Toboso*[2]
[1]*Chuo Kikuu cha Moi, Kenya*
[2]*Chuo Kikuu Kishirikishi cha Alupe, Kenya*

**Ikisiri**

**Kwa muda mrefu, lugha imekuwa ikitambulika kama ala ya kimsingi ya kufikiria, kufanikisha mawasiliano, kutambulisha, kuwasilisha utamaduni na katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, maendeleo ya kisiasa na uvumbuzi wa teknolojia mpya za mawasiliano ulimwenguni yameleta mielekeo mipya katika matumizi ya lugha. Sasa, lugha inatumiwa kwa njia zinazoidhihirisha na kuibainisha kama silaha ya kudhuru au hata kuangamiza. Katika historia ya mataifa, lugha imetumiwa katika maeneo mbalimbali katika kuanzisha vita, kuhujumu na hata kushawishi watu kufanya uhalifu. Kuzuka kwa intaneti kumesababisha kuibuka kwa mielekeo mipya ya usilahaishaji wa lugha. Majukwaa ya Twitter, Facebook, Instagram, Telegram na Whatsapp yamewapa watumizi wa mitandao hii fursa ya kutumia lugha kwa njia za kibunifu na kusababisha usilahaishaji wa lugha kwa njia za kipekee. Tafiti zimefanywa kuhusu uhalifu wa mitandaoni. Hata hivyo, suala la lugha na usilahaishaji wake halijashughulikiwa kwa dhati na kwa umuhimu unaostahili. Makala haya yanashughulikia usilahaishaji wa lugha katika majukwaa ya mitandao ya kijamii. Imebainika kwamba uhuru wa matumizi ya lugha katika mitandao hii umesababisha matumizi mabaya ya lugha.**

**Maneno Muhimu**: Usilahaishaji, Lugha, Intaneti, Teknolojia.

## Utangulizi

Uhalifu katika maisha ya wanadamu ni mkongwe jinsi historia yake ilivyo. Hata hivyo, uvumbuzi wa teknolojia ya kielektroniki na mitandao iliyofuatia ulipeleka uhalifu katika awamu mpya. Anavyosema Krone (2003) msimu wa kidijitali umejenga mazingira mapya kwa wahalifu. Mathalani, mhalifu aliye nchini Urusi anaweza kutekeleza uhalifu nchini Kenya na kuhamisha pesa kutoka benki ya Kenya hadi akaunti ya Uhispania huku akitumia sava iliyo nchini Uswizi. Suala la usialahaishaji lugha limeepuka diskosi za kitaaluma kwa muda mrefu. Suala

lililozungumziwa kwa muda sasa ni lile la ubwamelifu. Katika upana wake, ubwamelifu ni dhana inayorejelea uhalifu wa mitandaoni. Hudley na Anderson (2001) wanafasiri ubwamelifu kama uhalifu unaotekelezwa kwa kutumia tarakilishi. Ubwamelifu hufanikishwa na programu maalum za tarakilishi zilizowezeshwa kwa njia mahususi. Kumar (2002) anataja mitambo ya pesa ya mabenki na akaunti za benki, kadi za mikopo ya benki, uhamishaji wa kielektroniki wa pesa na biasharishi kama sekta zilizoathirika mno na ubwamelifu. Kuna pia na visa vya udukuzi wa kuiba huduma za simu kwa kunyakua muda wa mawasiliano ya makampuni (tazama Schiek, 1995; Tendler na Nuttal, 1996; Newman, 1998).

Visa vya matumizi ya ubwakameme (jumla ya mitandao ya kimataifa iliyosukwa pamoja na inayotumia tarakilishi, rununu na inayotumiwa kama mbinu ya mawasiliano, ghala la kuhifadhi maarifa) kutekeleza uhalifu vimechangia kuongezeka kwa uhalifu kama vile wizi wa vifaororo (Meyer na Underwood 2004), ulanguzi wa mihadarati, ulanguzi wa pesa na ulanguzi wa wanadamu. Kadhalika, ponografia ya watoto imerahisishwa na ubwakameme (Grant, David na Grabosky 1997; Grabosky, 2000). Tatizo la ubwamelifu lilisababisha bunge la Kenya kupitisha mswada wa Tarakilishi na Ubwamelifu, 2018, uliolenga kukabili uhalifu wa mitandaoni. Mswada huo ulitiwa saini na Rais Kenyatta na kuwa sheria mnamo Mei 16, 2018 (tazama gazeti la *Daily Nation,* Jumatano, Mei 16, 2018, Mei 26, 2018, Aprili 15, 2018). Sheria hii inahalalisha uhalifu wa aina yote unaotekelezwa kwa kutumia tarakilishi.

Kila aina ya uhalifu huwa na silaha au zana zake za kuufanikisha. Ubwamelifu hutekelezwa kwa kutumia tarakilishi. Tarakilishi nazo hutekeleza matendo kwa kufuata amri kutoka kwa wanadamu. Mawasiliano kati ya wanadamu na tarakilishi hufanikishwa na programu maalumu zilizo ndani mwa kila tarakilishi, na ambazo hutegemea lugha. Hii ina maana kwamba ili tarakilishi kutekeleza tendo fulani, lazima kuwe na mawasiliano ya kilugha kati ya mwanadamu na tarakilishi husika. Usemezano huu huwezesha tarakilishi na wanadamu kufikia mwafaka na kuwezesha tarakilishi kufanya uamuzi kuhusu tendo la kutekelezwa baada ya kutafakari na kuchuja matendo mengi yaliyo katika programu zake.

Hali kwamba tarakilishi hutegemea mawasiliano ya kilugha ili kutenda uhalifu inaifanya lugha kuwa silaha na wenzo wa kufanikisha uhalifu unaotegemea tarakilishi. Kwa sababu hii, lugha ni silaha ya kufanikisha ubwamelifu. Nafasi ya lugha katika kuwezesha ubwamelifu inadhihirika katika sheria mpya ya Tarakilishi na Ubwamelishi nchini Kenya. Mathalani, sheria hii inaharamisha uchapishaji na usambazaji mitandaoni wa habari zisizo za kweli. Sheria hii ilitungwa kutokana na visa vya ubwamelifu vilivyoshamiri katika mitandao inayohusisha Wakenya. Sheria hii imelenga kuangaza ujumbe na maudhui katika mawasiliano ya mitandaoni hususan mitandao ya kijamii. Kwa

kufanya hivi, sheria hii inaashiria kwamba lugha inayotumiwa katika mawasiliano ya kibwamelifu inatumiwa kama silaha ya kufanikisha uhalifu.

## Mitindo ya Usilahaishaji Lugha

### Uvizindao (*Cyberstalking*)

Uvizindao ni silaha maarufu ya kuogofya wapinzani. Uvizindao unaweza kufasiriwa kama matumizi ya mitandao au vifaa vya kielektroniki ili kumvizia mtu, kundi la watu au shirika. Akdeniz (1999) anaufasiri uvizindao kama hali ya kuendelea kumtumia mtu ujumbe asiotaka. Uviziaji katika hali hii hutekelezwa kwa nia isiyo njema. Katika visa vilivyotokea, uzivindao umetekelezwa kwa malengo anuwai kama kutoa madai ya uongo, kuchokoza kuharibia mtu sifa, kuhujumu, kupeleleza shughuli za kisiri za mtu au kulemaza shughuli zake. Uvizindao ni tendo la kihalifu. Kwa kuwa uvizindao hutegemea lugha kama ala ya kuufaulisha, lugha hiyo huchukua nafasi ya silaha hatari ya kimtandao. Katika kufanikisha uhalifu huu, mhusika husaka mtu mwingine mtandaoni na kumtumia ujumbe ulio na nia ya kumtisha ama kuhujumu shughuli zake. Mitandao inayotumiwa katika uvizitandao ni kama vile Kitandazi, Instagramu, Mesenja na WhatsApp. Uvizindao pia hutekelezwa katika jumbe fupi za simu na barua pepe.

Kati ya mitandao hii, Kitandazi, Twitter na WhatsApp ndiyo inatumiwa zaidi. Hali hii inatokana na sababu kwamba hii ni mitandao maarufu iliyo na mamilioni ya watumizi. Kwa sababu hii, waviziaji hupata urahisi wa kusaka kurasa za waviziwa. Kadhalika, hii ni mitandao ya kimataifa ambayo haiathiriwi na sera za lugha au za mawasiliano za mataifa binafsi. Kwa hivyo, watumizi wa mitandao hii huteua lugha bila kujali sera za mataifa yao. Hali hii imefanya uvizindao kukosa mipaka ya kimataifa. Uvizindao katika Kitandazi ni tata. Sababu ni kwamba mwasilianaji asiye rafiki wa mitandaoni anaweza kufikia ukurasa wa mwenziwe wa mawasiliano kupitia kwa huduma ya usambazaji wa ujumbe wa marafiki. Kupitia kwa huduma hii, mtu anaweza kuvizia ukurasa wa hasimu yake na kuandika ujumbe. Upenyu huu ndio hutoa nafasi kwa usilahaishaji lugha. Mitandao mingi pia huwapa watumizi fursa ya kujisajili kwa kutumia majina bandia. Kwa sababu hii, watumizi huvizia mahasimu na kuomba kuwa marafiki zao bila mahasimu walengwa kugundua. Hii huwapa fursa ya kutuma ujumbe wenye lugha iliyosilahaishwa.

### Wigonafsi (*Impersonation*)

Hapa, tunazungumzia nafasi ya lugha katika wigonafsi. Wigonafsi katika intaneti hutumiwa kama zana ya kivita. Hii ni mbinu ya kuchukua nafsi ya mtu mwingine bila idhini yake kwa kutumia jina lake au picha yake ili kumwangamiza. Aghalabu, mviziaji hujifanya mtu huyo kwa kutumia nafsi yake. Nia ya wigonafsi huwa ni kuchokoza, kuhujumu, kuharibia sifa au kulemaza shughuli za mtu. Lugha hutumika katika wigonafsi kwa njia anuwai. Kwanza, katika kutoa

maagizo kwa tarakilishi ili kupenya kurasa za mitandao ya watu wengine. Pili, kama njia ya kutuma ujumbe kwa kurasa za mitandao zilizobuniwa kwa kutumia jina la mtu fulani. Hii ni mbinu maarufu inayotumiwa katika mitandao kutimiza malengo ya kiuchumi, kisiasa au kihalifu. Wigonafsi katika mitandao ya kijamii huhusu kunyakua kwa kurasa za watu binafsi na kujifanya wenye kurasa hizo. Mwigaji nafsi huweza kuwasiliana na marafiki wa mwenye ukurasa huo bila idhini yake na wakati mwingi kuzua uhasama. Dhamira ya kufanya hivi huwa kumharibia mwenye ukurasa huo sifa au kuleta uhasama. Mitandao maarufu inayotumiwa mno ni Kitandazi, Whatsapp, Twita na mitandao ya mawasiliano ya kiuchumi kama M-Pesa nchini Kenya. Mathalani, katika mitandao ya M-Pesa wahalifu hujifanya wahudumu wa kampuni ya M-Pesa na kutuma jumbe unaolenga kutapeli. Wigo nafsi pia hurejelea hali ya kubuni kurasa za mitandao kwa kutumia majina ya watu wengine, kwa nia ya kuwadhulumu. Tazama mfano ufuatao:

Nambari ya simu ya mtumaji

Mfano

Dear Customer

M-AKIBA LOAN is Now available,

From:

10,000/=

20,000/=

50,000/=

100,000/=

Loan payment: 5 To 20 months

CALL SMS: SMS 5555555555

0794………..

Mfano huu unaonyesha ujumbe tuliotumiwa na mtu aliyechukua nafsi ya kampuni ya M-Akiba. Mtumaji wa ujumbe alijifanya afisa wa kampuni hii akiwa na nia ya kutapeli. Inadhihirika hapa kwamba lugha katika ujumbe huu imesilahaishwa ili kuwa silaha ya kujinyakulia nafsi ya kampuni ya M-Akiba Loan. Unyakuzi wa nafsi ni hatia na katika hali hii ulilenga kushawishi kwa nia ya kutapeli.

**Vitabwame (*Cyber warfare*)**

Dhana ya vitabwame ina maana anuwai. Kwanza, hurejelea hujuma kwa vifaameme vya wapinzani au mahasimu hususam vile vya kitarakilishi. Hujuma hii hutekelezwa kwa kutumia programu maalum za kitarakilishi au kirusilishi. Tunaweza pia kusema kwamba haya ni mashambulizi ya tarakilishi kwa tarakilishi nyingine. Nia huwa kuharibu mitambo ya tarakilishi ya wapinzani au

mahasimu ili kulemaza shughuli za watu hao. Hujuma hizi pia zinaweza kutekelezwa kwa nia ya kuiba ujumbe au maarifa muhimu yaliomo katika tarakilishi zinazolengwa. Pili, vitabwame hurejelea ushindani wa mitandaoni ambao huchukua mtindo wa kivita. Vitabwame ni maarufu katika vita vya silaha kati ya mataifa. Vita hivi huhusu mashambulizi kwa silaha zinazotumia tarakilishi kama meli za kivita, ndege, mizinga nk. Hata hivyo, vitabwame pia ni mbinu inayotumiwa katika mapambano ya kiuchumi na kisiasa. Vita katika mkondo huu huhusisha mashambulizi kwa vifaameme vya makampuni shindani ya kibiashara au tarakilishi za wapinzani wa kisiasa. Nchini Kenya, kumekuwa na lawama kati ya wanasiasa kuhusu wizi wa kura wa miaka ya 2007, 2013 na 2017 ambao unadaiwa kutekelezwa kivitameme.

Aina zote mbili za vitabwame huhitaji lugha kama malighafi ya ufanisi wake. Katika mashambulizi ya vifaameme, lugha hutumiwa ili kutoa maagizo kwa tarakilishi zinazoshambuliwa au kuhujumiwa. Programu za kutumika katika mashambulizi ya tarakilishi hutumia lugha iliyosilahaishwa. Lugha hii huwa silaha ya kupenya tarakilishi za wapinzani na mahasimu na kuziharibu, kuzizima au kuiba maarifa na ujumbe. Lugha pia huwa silaha ya kubadilisha ujumbe uliomo na kupandikiza mwingine. Lugha hiyo hurahisisha usemezano kati ya tarakilishi ya kushambulia na ile ya kushambuliwa. Lugha ya vita mitandaoni imetumiwa katika ushindani wa kibiashara na kisiasa. Mathalani, wafanyibiashara hutumia mitandao kushambulia washindani wao katika biashara. Wanasiasa hutumia mitandao kushambulia washindani wao. Mitandao ya blogu ndiyo hutumiwa zaidi kwa kuwa blogu huruhusu maandishi marefu. Mitandao ya Twitter na Kitandazi nayo imekuwa maarufu katika vita bwame kwa kuwa inafikia watu wengi.

## Upujufu na Ponografia

Upujufu na ponografia kama silaha ya mitandaoni imekuwa maarufu. Upujufu unaweza kufasiriwa kama matumizi ya lugha ya aibu hasa ile inayotaja au kuashiria masuala ya ngono. Nia huwa kuaibisha au kumlazimu mwenye mtandao kuufunga. Ujumbe wenye lugha pujufu hutumwa katika kurasa za mahasimu hasa wale wa kibiashara au kisiasa au mahasimu. Kwa njia hii, upujufu na ponografia hutumika kama zana ya kivita. Hata hivyo, watu wasio katika biashara wala siasa pia hushiriki. Aghalabu, lugha ya upujufu huandamana na grafolojia yenye mvuto kama video, michoro, picha na herufi zenye fonti kubwa. Mathalani, picha na video hutumwa katika kurasa za mahasimu baada ya kurasa hizo kudukuliwa. Upujufu hutumiwa kama njia ya kushambulia mahasimu na kuwatia aibu. Picha za ponografia zinapowekwa katika kurasa za wapinzani za Facebook na Twita, hutumika kama silaha ya kuaibisha na kudhalilisha. Kadhalika, hutumiwa kama silaha ya kufukuza marafiki wa mlengwa kutoka katika ukurasa wake. Kwa kuwa

upujufu na ponografia ni zana za kivita, lugha inayotumiwa katika kuwezesha zana hizi pia huwa silaha.

**Vitisho**

Vitisho ni zana ya kivita inayotumiwa katika siasa na uchumi. Lugha tishi ni maarufu katika mawasiliano ya kawaida kama yale ya ana kwa ana nay ale ya kimaandishi. Utandawazi na kuzuka kwa mitandao ya mawasiliano ya kielektroniki kumetoa nafasi ya kupanuka kwa matumizi ya lugha hii ambayo sasa imeenea na kuwa maarufu katika intaneti. Mathalani, baadhi ya watumizi wa mitandao wamebuni mbinu za kutumia lugha kufanikisha malengo ya kuwadhoofisha mahasimu wao kwa kuwavamia, kuwashambulia na kuhujumu shughuli zao hasa zile za lainini. Katika misingi hii, lugha imetumiwa kama silaha ya kutimiza malengo ya kuzua uoga. Ni muhimu kukumbuka kwamba katika vita, silaha kubwa na hatari hubuniwa na kutumiwa kuwili. Kwanza, kama njia ya kushambulia mahasimu na kuwaangamiza kabla hawajakushambulia. Pili, silaha hutumiwa kama kigingi cha kutisha na kuzima mipango ya mahasimu ya kukushambulia. Katika hali hii, silaha haitumiki moja kwa moja bali uwepo wake huwa kizuio kwa mashambulizi ya mahasimu. Silaha hizo huwaogofya mahasimu na kufifisha mipango yao ya mashambulizi, kwa mfano:

> Watu wanatembea na mahaby za wengine, haki will chop off your pussy ya mtu.

Mfano huu unadhihirisha mwasilianaji wa Kitandazi ambaye anamtisha mwenziye ambaye hajamtaja. Haibainiki hata hivyo, iwapo mtishwa ni rafiki yake wa Facebook. iwapo ni rafiki wa Kitandazi, basi kuna uwezekano kwamba vitisho hivyo vilimfikia. Ni muhimu pia kutaja kwamba hata bila ya ujumbe huu kumfikia mlengwa, lugha iliyomo inatisha na imetumika kama silaha hatari. Lugha iliyomo inaogofya kwa kuwa mwasilianaji anatisha kumkata hasimuye sehemu za siri (chop off your pussy). Lugha hii imelenga kum(wa)nyamazisha hasimu, kumwogofya na kusimamisha matendo yanayoshukiwa. Kadhalika, lugha imetumika kama kizuio kwa wale wanaoshukiwa kupanga kutekeleza tendo hilo.

**Matusi**

Mitandao imekuwa jukwaa la kutumia matusi kama zana ya kivita. Hali hii inatokana na uhuru wa kimawasiliano katika mitandao hii. Hali kwamba matumizi ya lugha katika mitandao hii hayadhibitiwi na kwamba mitandao mingi ni ya kimataifa na haidhibitiwi na sheria za taifa lolote moja inaipa mitandao hii uhuru unaotumiwa vibaya na wawasilianaji. Uhuru huu ndio unaotumiwa na wawasilianaji kurusha matusi kwa mahasimu na wapinzani. Mathalani, nchini Kenya, kurasa mpya za Blogu, Facebook na WhatsApp huzuka katika msimu wa siasa. Kurasa nyingi huanzishwa kwa lengo la kampeni za kisiasa. Kwa sababu ya upinzani wa kisiasa, kurasa hizi huwa na majibizano yaliyo na matusi. Kurasa

za magazeti hususan zile zilizo na habari za kisiasa pia huwa na moni ya mashabiki yaliyo na matusi. Hii ina maana kwamba watumizi wa mitandao hutumia majukwaa ya makampuni ya habari kuwadhalilisha kimatusi wapinzani wao hasa wale wa kisiasa.

**Wizibwame (*Cybertheft*)**

Wizibwame kama silaha hasa hutumiwa katika siasa. Njia maarufu ya wizibwame ni wizi wa data inayotumiwa kudhoofisha wapinzani wa kisiasa na mahasimu. Wizibwame, kadhalika, hutumiwa kama silaha ya kufanikisha ufisadi. Imebainika sasa kwamba watu fasidi wanatumia mitandao kuendeleza shughuli zao. Hii inatokana na hali kwamba mawasiliano ya mitandaoni na shughuli za intaneti haziwezi kufwatiliwa kwa urahisi. Hali ya faragha katika intaneti na habari nyingi zilizo katika mitandao ya intaneti zimejenga mazingira mwafaka kwa wafisadi kuendesha shughuli zao bila kugunduliwa. Mathalani, kumekuwa na madai kwamba wakati wa kura za Kenya za mwaka wa 2017, kampuni ya *Cambridge Analytica* ilitumia mtandao wa Facebook kuiba data kuhusu maoni ya kisiasa ya Wakenya. Data hii ilitumiwa kubuni mikakati ya kisiasa iliyotumiwa katika kampeni. Kampuni hii pia imedaiwa kutumia mikakati kama hiyo wakati wa kampezi za Marekani za mwaka wa 2017. Hali hii inaonyesha jinsi mitandao inatumiwa kama silaha ya kuendeshea ufisadi.

**Udukuzi**

Udukuzi ni hali ya kuingia katika mitandao au mawasiliano ya watu wengine kisirisiri ili kukwamiza shughuli zao au kutekeleza wizi. Kwa hivyo, udukuzi mitandaoni hutumiwa kama zana ya kivita. Teknolojia maalum hutumiwa ili kuvizia mitandao au mawasiliano yaliyolengwa kuviziwa. Udukuzi mwingine hufanywa ili kupindua mawasiliano ya mtu fulani ili yaelekezwe kwa mtu mwingine. Kumekuwa pia na visa vya udukuzi wa kuiba huduma za simu kwa kunyakua muda wa mawasiliano ya makampuni (Schiek, 1995; Tendler na Nuttal, 1996; Newman, 1998). Kwa hivyo, chanzo cha udukuzi ni lugha iliyomo katika mitandao au mawasiliano yanayodukuliwa.

Lugha hutumiwa katika udukuzi kama silaha ya mchakato wa udukuzi ili kupata habari. Mchakato wa udukuzi hutegemea tarakilishi. Tarakilishi nazo hutegemea maagizo ambayo hutolewa kwa kutumia lugha hususan zile za mawasiliano mapana. Utegemezi wa lugha katika mchakato huu ndio unaosilahaisha lugha. Baadhi ya wadukuzi huingia katika mitambo ya tarakilishi kama ile ya benki ili kuiba pesa. Wadukuzi wengine hutuma habari kwa watu wenye mitambo ya kudukuliwa na kuwaelekeza kufuata utaratibu fulani ili kufungulia wadukuzi kurasa zao za mawasiliano na akaunti za benki bila wao kujua. Kurasa hizi zikisha kufunguliwa, habari muhimu zilizomo huibwa. Mitandao inayolengwa mno hapa ni kama email, Facebook, Twitter, Instagram nk. Kadhalika, lugha katika habari zinazopatikana kupitia kwa udukuzi hutumiwa

kama silaha ya kupambana na wapinzani hasa wa kisiasa na kiuchumi. Lugha ya habari zinazodukuliwa hutumiwa pia kama silaha ya propaganda na hata ya utapeli.

Nchini Kenya, visa vya udukuzi wa mitamdao Laini ya pesa vimeshamiri. Visa hivi vimeathiri mitandao kama vile M-Pesa. Pia kumekuwa na visa vya wanafunzi hasa wa vyuo vikuu kudukua tarakilishi za vyuo vikuu uli kuiba mitihani au kubadilisha alama zao. Udukuzi unaoathiri mitandao ya kijamii kama Kitandazi huhusu kupaka tope kurasa za watu binafsi. Hili hutekelezwa kwa kudukua kurasa hizo na kutuma picha za ponografia au ujumbe mchafu.

**Propaganda**

Visa vya propaganda katika mitandao vimekuwa vingi. Propaganda katika mitandao huenezwa na watu binafsi, makampuni ya kibiashara na hata wanasiasa. Propaganda huwa umbea au habari za uzushi kuhusu mtu, kundi la watu, serikali au shirika. Wakati wa uchaguzi wa Marekani wa mwaka wa 2017, mgombezi mmoja, Trump alilaumu wapinzani wake na vyombo vya habari kwa kueneza umbea kumhusu. Wakati wa uchaguzi wa nchini Kenya wa mwaka wa 2017, mitandao mingi ilibuniwa katika Facebook ili kueneza propaganda. Makampuni ya utafiti yalitumiwa na wanasiasa kufanya utafiti na kueneza habari za uongo kuhusu wapinzani. Lugha inayotumiwa katika propaganda huwa yenye mvuto mkubwa ili kuweza kufanikisha malengo yake kama silaha. Kadhalika, lugha hii huwa na uhusiano na hali halisi kumaanisha kwamba waenezaji wa propaganda hufanya utafiti kuhusu mlengwa ili kujua mambo yanayomhusu ambayo yakienezwa yanaweza kuaminiwa kuwa ni ukweli. Wasomaji wa habari hizo huamini propaganda zinazoenezwa. Kinachowafanya kuamini hivi ni usilaha wa lugha iliyotumiwa.

***Blackmail e.g. YouTube***

Huu ni mtindo unaohusisha kuangikwa kwa video au picha za mwathiriwa katika You Tube ili kuwaharibia sifa. Mtindo huu hutumiwa na mahasimu wa kisiasa na kiuchumi kuwaharibia sifa wapinzani wao. Mtindo huu pia hutumiwa na matapeli wa kiuchumi kuwakandamiza walengwa. Katika hali hii, picha za video huandamana na maneno yaliyozungumzwa na mlengwa katika muktadha tofauti ili kuonekana kwamba yalisemwa katika muktadha wa video hiyo. Kumekuwa pia na visa vya video za utupu zilizoandamana na maneno ya mwathiriwa ambayo yamefanyiwa uhariri ili kuaminika kwamba yalisemwa katika muktadha wa video hiyo. Video nyingine zimeandamana na maneno yaliyosemwa na mtu mwingine lakini aliye na sauti kama ya mwathiriwa. Kusudi la lugha katika video hizi huwa kukandamiza, kunyamazisha, kuaibisha, kulazimu mtu kubadili mipango yake au hata kumwibia.

## Hitimisho

Kwa muda mrefu, lugha imekuwa ikitambulika kama ala ya kimsingi ya kufikiria, kufanikisha mawasiliano, kutambulisha, kuwasilisha utamaduni na katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Hata hivyo, maendeleo ya kisiasa na uvumbuzi wa teknolojia mpya za mawasiliano ulimwenguni yameleta mielekeo mipya katika matumizi ya lugha. Sasa, lugha inatumiwa kwa njia zinazoidhihirisha na kuibainisha kama silaha ya kudhuru au hata kuangamiza. Katika historia ya mataifa, lugha imetumiwa katika maeneo mbalimbali katika kuanzisha vita, kuhujumu na hata kushawishi watu kufanya uhalifu. Kuzuka kwa intaneti kumesababisha kuibuka kwa mielekeo mipya ya usilahaishaji wa lugha. Majukwaa ya Twita, Facebook, Instagram, Telegram na Whatsapp yamewapa watumizi wa mitandao hii fursa ya kutumia lugha kwa njia za kibunifu na kusababisha usilahaishaji wa lugha kwa njia za kipekee.

## Marejeleo

Munde, J. (2018). President Kenyatta assents to Cybercrimes Bill amid protests. Daily Nation, May 16, 2018.

Kiprono, D. (2018). Kenya needs Comprehensive Cybercrime Law. Gazeti la *Daily Nation* Aprili 14, 2018.

Newman, K. (1998). Phone call scams skim of millions. *New Zealand Herald* August 8, 1998.

Tendler, A. na Nuttal, N. (1996). Hackers leave Red Faced yard with bill. *The Australian*, Agosti 6, ukur 37

Kumar, A. (2002). *Cybercrime- crime without punishment*. Imepakuliwa kutoka www.inomy.com

Grant, A, David, F. na Grabosky, P. (1997). *Transnational organized crime*. Vol 3, No 4.

London: Frank Cass and ccccompany.

Meyer, M. na Underwood, A. (1994). *Crimes of the West. Newsweek,* November 15, 1994, kur 68.